TANGAZO LA SERIKALI Na. 313 lililochapishwa tarehe 31/07/2015

SHERIA YA DAWA NA VIFAA TIBA,
(SURA 219)

KANUNI

(Zimetengezwa chini ya kifungu cha 122 (1) (x), (z))

KANUNI ZA UONDOAJI KATIKA SOKO, USHUGHULIKIAJI NA UTEKETEZAJI WA DAWA ZISIZOFAA, 2015

MPANGILIO WA KANUNI

Kanuni *Jina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

1. Jina
2. Matumizi
3. Tafsiri

SEHEMU YA PILI
UONDOAJI KATIKA SOKO

4. Katazo la kuuza dawa zilizoamriwa kuondolewa katika soko
5. Uondoaji dawa katika soko
6. Utoaji taarifa ya kuondoa dawa katika soko
7. Tathmini ya athari za kiafya
8. Aina za uondoaji wa dawa katika soko

SEHEMU YA TATU
USHUGHULIKIAJI NA UTEKETEZAJI WA DAWA ZISIZOFAA

9. Katazo la kuteketeza dawa zisizofaa
10. Uamuzi wa kuteketeza dawa zisizofaa
11. Ombi la kuteketeza dawa zisizofaa
12. Idhini ya kuteketeza dawa zisizofaa
13. Ushughulikiaji wa dawa zisizofaa

14. Uteketezaji wa dawa zisizofaa

SEHEMU YA NNE
MASHARTI YA JUMLA

15. Pingamizi
16. Rufaa
17. Makosa na adhabu
18. Kufifilisha makosa

MAJEDWALI

SHERIA YA DAWA NA VIFAA TIBA,
(SURA 219)

KANUNI

(Zimetengezwa chini ya kifungu cha 122 (1) (x), (z))

KANUNI ZA UONDOAJI KATIKA SOKO, USHUGHULIKIAJI NA UTEKETEZAJI WA DAWA ZISIZOFAA, 2015

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Uondoaji katika Soko, Ushughulikiaji na Uteketezaji wa Dawa zisizofaa, 2015.

Matumizi

2. Kanuni hizi zitatumika katika kuondoa, kushughulikia na kuteketeza dawa zisizofaa ndani ya Tanzania Bara.

Tafsiri

3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa muktadha unahitaji vinginevyo:

Sura 219

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba;

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba au kwa kifupi TMDA iliyoundwa chini ya kifungu namba 4 (1) cha Sheria;

"uteketezaji" maana yake ni utaratibu wa kutoa dawa zisizofaa katika kazi zake za kibailojia na kemikali ili zisiwe na athari;

Sura 191

"Mkaguzi wa mazingira" maana yake ni mkaguzi aliyeteuliwa kwa mujibu wa kifungu cha 82 cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"Mkaguzi" maana yake ni mkaguzi aliyeteuliwa, aliyeidhinishwa au kutambuliwa chini ya Sheria;

"mwingizaji" maana yake ni mtu au taasisi iliyoidhinishwa chini ya Kanuni hizi kuingiza dawa kwa lengo la kuuza, kugawa kwa kuuza, kusambaza, kutoa msaada au kutumika Tanzania;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya afya kwa wakati huo;

"Dawa" maana yake ni dawa kama ilivyotafsiriwa kwenye Sheria;

"Kuondoa katika soko" maana yake ni kuondoa dawa katika soko kwa sababu zinazohusiana na upungufu wa ubora, usalama au ufanisi;

"msimamizi" maana yake ni mfamasia au daktari wa mifugo mwenye jukumu la

kusimamia uingizaji au usafirishaji nje ya nchi kama alivyosajiliwa chini ya Sheria ya Famasi au Sheria ya Mifugo;
"Dawa zisizofaa" maana yake ni dawa ambazo zimekwisha muda, zimefungashwa vibaya, zimeharibika, hazijamaliza muda wa matumizi lakini zimehifadhiwa vibaya, hazina lebo sahihi, bandia, duni, zimechakachuliwa, zimepigwa marufuku au hazijaidhinishwa na Mamlaka.

SEHEMU YA PILI
UONDOAJI KATIKA SOKO

Katazo la kuuza dawa zilizoamriwa kuondolewa katika soko

4.- Mtu yeyote hataruhusiwa kuuza au kusambaza dawa ambazo zimeamriwa au kuelekezwa kuondolewa katika soko.

Uondoaji dawa katika soko

5.- (1) Litakuwa ni jukumu la mmiliki au wakala wake wa dawa kuondoa dawa katika soko.

(2) Mamlaka yenyewe inaweza kuagiza dawa kuondolewa katika soko wakati wowote kwa sababu zinazohusiana na upungufu katika ubora, usalama au ufanisi kwa gharama ya mtengenezaji, mmiliki au mwingizaji.

(3) Kabla au wakati wa kuondoa dawa katika soko kama ilivyoainishwa katika kanuni ndogo ya (1), mtengenezaji, mmiliki au mwingizaji wa dawa atawasilisha taarifa zifuatazo kwa Mamlaka: -

(a) jina la biashara na jina halisi la dawa, muundo wa dozi, nguvu ya dawa, namba ya toleo au loti, ukubwa wa pakiti, jina na anuani ya mtengenezaji, tarehe ya kutengenezwa na tarehe ya kumaliza muda wa matumizi ya dawa;
(b) sababu ya kuondoa katika soko, uhalisia wa kasoro au uwezekano wa kasoro, tarehe na mazingira ya kasoro au uwezekano wa kasoro zilipobainika;
(c) jumla ya dawa zinazoondolewa katika soko ambazo awali zilimilikiwa na mtengenezaji, mmiliki au mwingizaji;
(d) tarehe ambayo usambazaji wa dawa ulianza;
(e) jumla ya dawa zilizoondolewa katika soko ambazo zilisambazwa hadi kufikia muda wa kuondolewa katika soko;
(f) maeneo ambako dawa zimesambazwa;
(g) orodha ya wateja ambao wamesambaziwa dawa; na
(h) idadi ya dawa inayoondolewa ambayo bado ipo kwa mmilki, mtengenezaji au mwingizaji

(4) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), mtengenezaji, mmiliki au

mwngizaji anaweza kuanzisha kwa hiari uondoaji wa dawa yoyote baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa watumiaji au baada ya uthibitisho wa uchunguzi kwamba dawa hiyo imesababisha au ipo karibu kusababisha madhara ya kiafya au kuhatarisha usalama wa wagonjwa, watumiaji au watu wengine.

(5) Mtengenezaji, mmiliki au mwingizaji ambaye ameanzisha kwa hiari uondoaji wa dawa katika soko chini ya kanuni ndogo ya (3) atahitajika kufuata masharti yaliyowekwa chini ya kanuni ndogo ya (2).

Utoaji taarifa ya kuondoa dawa katika soko

6.- (1) Mtengenezaji, mmiliki au mwingizaji atalazimika kuwasilisha kwa Mamlaka taarifa ya uondoaji wa dawa katika soko kila wiki na taarifa ya mwisho ya uondoaji, ikihusisha ulinganifu wa kiasi kilichosambazwa na kilichoondolewa.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), mtengenezaji, mmiliki au mwingizaji wa dawa atapaswa kuwasilisha kwa Mamlaka taarifa ya uchunguzi inayoeleza chanzo cha kasoro na hatua alizochukuwa katika kurekebisha na kuzuia kasoro hiyo kujirudia.

Tathmini ya athari ya kiafya

7.- (1) Tathmini ya athari ya kiafya iliyosababishwa na dawa iliyoondolewa katika soko au inayotarajiwa kuondolewa itafanywa na Mamlaka kwa kuzingatia vigezo mbalimbali ikiwemo vifuatavyo:

(a) iwapo itabainika kama kuna ugonjwa wowote au majeraha tayari yaliyotokea kutokana na matumizi ya bidhaa husika;

(b) iwapo itabainika kama kuna dalili zozote za kitabibu zinazoashiria athari ya kiafya kwa wanadamu au wanyama. Matokeo yoyote ya tathmini yatapaswa kuwa na uthibitisho wa kisayansi au nyaraka za maoni ya mtu aliyefanya tathmini au uamuzi.

(c) tathmini ya athari kwa makundi ya watu, kama vile, watoto, wagonjwa waliofanyiwa upasuaji, mifugo na wanyama pori, pamoja na makundi mengine ambayo yanaweza kuathiriwa na dawa husika, hususani wale wanaoweza kupata athari kubwa kwa haraka.

(d) tathmini ya kiwango cha ukubwa wa athari ya kiafya kwa makundi ya jamii yanayoweza kuathiriwa kwa urahisi;

(e) tathmini ya uwezekano wa kutokea kwa athari; na

(f) tathmini ya matokeo ya athari za haraka au muda mrefu.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), Mamlaka itatenga makundi ya kuondoa dawa katika daraja la I, daraja la II, au daraja la III, kulingana na uhusiano wa kiwango cha athari ya kiafya kwa dawa inayoondolewa au kutarajiwa kuondolewa katika soko.

Aina za uondoaji wa dawa katika soko

8 .- (1) Kutakuwa na aina tatu za madaraja ya kuondoa dawa katika soko kama ilivyoainishwa katika Kanuni hii kulingana na athari ya kiafya au matukio yatokanayo na madhara ya dawa-

(a) Daraja la I ni kwa ajili ya dawa zenye kasoro, hatarishi au

zinazoweza kutishia maisha ya binadamu au mifugo na zinaweza kutabirika au kusababisha athari kubwa ya kiafya, matukio mabaya au kifo;

(b) Daraja la II ni kwa ajili ya dawa ambayo inaweza kusababisha athari ya muda au shida ya kiafya inayoweza kurekebishika au kushindwa kutibu.

(c) Daraja la III ni kwa ajili ya dawa yenye kasoro na isiyo na uwezekano wa kusababisha athari yoyote ya kiafya au ambayo haikidhi matakwa ya Sheria ya masharti ya vifungashio vilivyochapishwa, viwango au uwekaji lebo.

(2) Muda wa kuondoa dawa katika soko kwa daraja la I, II na III hautazidi siku kumi na nne, ishirini na moja na thelathini mtawaliwa.

(3) Bila kujali kanuni ndogo ya (2), Mamlaka ina haki ya kuongeza muda wa kuondoa dawa katika soko kulingana na uharaka na hatari ya kiafya.

SEHEMU YA TATU
USHUGHULIKIAJI NA UTEKETEZAJI WA DAWA ZISIZOFAA

Katazo la kuteketeza dawa zisizofaa

9.- Mtu yeyote hataruhusiwa kuteketeza dawa yoyote isiyofaa isipokuwa akiomba na kupewa idhini na Mamlaka kuendelea na utaratibu wa kuteketeza.

Uamuzi wa kuteketeza dawa zisizofaa

10.- Uamuzi wa kuanzisha uteketezaji wa dawa zisizofaa utapaswa kufanywa na Mamlaka, Mfamasia wa Mkoa, Wilaya au Hospitali, Mmiliki au Msimamizi wa kituo au jengo, Msimamizi au Mkaguzi.

Ombi la kuteketeza dawa zisizofaa

11.- (1) Ombi la kuteketeza dawa zisizofaa litawasilishwa kwa Mamlaka kwa kujaza fomu iliyoainishwa katika **Jedwali la Kwanza** la Kanuni hizi.

(2) Ombi litapaswa kuambatana na orodha ya dawa inayoonesha jina la biashara, jina halisi, nguvu na muundo wa dozi pale inapofaa, aina ya kifungashio, ukubwa wa pakiti, idadi, jina la mtengenezaji, namba ya toleo au loti na thamani ya kila dawa kwa bei ya soko.

Sura. 348

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1) na (2), ombi la kuteketeza dawa zisizofaa kutoka Taasisi za serikali litaambatana na idhini kutoka kwa Msajili wa Hazina ikionesha kwamba dawa hizo zimefutwa na kwamba zinaweza kutekeketezwa kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Umma.

Idhini ya kuteketeza dawa zisizofaa

12.- (1) Mamlaka itapokea ombi la kuteketeza dawa na itateua mkaguzi wa kuhakiki au kuthibitisha taarifa iliyowasilishwa kuhusiana na shehena inayoombewa kuteketezwa.

(2) Uthibitishaji unaotajwa katika kanuni ndogo ya (1) utafanywa kwa kutumia Fomu iliyoainishwa katika **Jedwali la Pili** la Kanuni hizi

(3) Mamlaka baada ya zoezi la uhakiki, itamjulisha mwombaji kuwasiliana na

taasisi ya Serikali yenye dhamana ya usimamizi wa mazingira kuhusu njia sahihi ya uteketezaji ambayo itatoa kibali cha kuteketeza.

(4) Mwombaji atawasilisha kwa Mamlaka cheti cha kuruhusu kuharibu dawa kutoka taasisi yenye dhamana ya usimamizi wa mazingira na atawasiliana na Mamlaka ya Serikali za Mitaa au matanuru yaliyoidhinishwa kwa ajili ya kuteketeza.

(5) Gharama za uteketezaji zitalipwa na mmiliki wa shehena.

Ushughulikiaji wa dawa zisizofaa

13.- (1) Mtu yeyote hataruhusiwa kuuza, kusambaza, kugawa au kuonesha kwa lengo la kuuza, kumiliki dawa zisizofaa.

(2) Wauzaji wa dawa watazingatia masharti yafuatayo-

(a) kutunza rejesta ya dawa zisizofaa kwa kutumia fomu iliyoainishwa katika **Jedwali la Tatu** la Kanuni hizi;

(b) kutenganisha dawa za tiba zenye asili ya kulevya, dawa za saratani, vijiuasumu na dawa nyingine yoyote hatarishi;

(c) kuweka kwa makundi dawa zisizofaa kwa kuzingatia miundo ya dozi zake-

i. yabisi, nusu-yabisi na poda: vidonge, poda za sindano, kapsuli, chembechembe, krimu, mishumaa ya jeli;

ii. vimiminika: majimaji, ya kuchanganya, sirapu, michanganyiko, losheni, erosoli na ya njia ya hewa,

(d) kutenga eneo la kuweka dawa zisizofaa lililoandikwa wazi kwa wino mwekundu kwa maneno "Hazifai kwa matumizi"; na

(e) kutunza dawa zisizofaa katika hali ya usalama katika jengo lililosajiliwa hadi hapo zitakapoteketezwa.

Uteketezaji wa dawa zisizofaa

14.- (1) Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi, Mkaguzi, Afisa Afya, Mkaguzi wa Mazingira, Askari Polisi au afisa mwingine aliyeidhinishwa watasimamia usafirishaji wa shehena kutoka katika jengo kwenda katika eneo la kuteketezea dawa.

(2) Uteketezaji wa dawa utasimamiwa na Mkaguzi, Afisa Afya Mkaguzi wa Mazingira, Askari Polisi au afisa mwingine aliyeidhinishwa na baada ya kukamilisha, wasimamizi na mmiliki wa shehena au mwakilishi wake kwa pamoja watasaini fomu ya uteketezaji kama ilivyoainishwa katika **Jedwali la Nne** la Kanuni hizi.

(3) Mamlaka, baada kupokea fomu ya uteketezaji wa dawa itatoa cheti cha kuteketeza dawa zisizofaa kama ilivyoainishwa katika **Jedwali la Tano** la Kanuni hizi.

SEHEMU YA NNE
MASHARTI YA JUMLA

Pingamizi

15. -(1) Mmiliki, mwingizaji au mtengenezaji wa dawa ambaye haridhiki na maamuzi yaliyotolewa na Mamlaka kuhusu kuondoa dawa katika soko au kuteketeza dawa zisizofaa anaweza kuwasilisha pingamizi lake akieleza sababu za kupinga maamuzi ya Mamlaka kwa maandishi kwa Mkurugenzi Mkuu au mtu yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi Mkuu kumwakilisha.

(2) Taarifa ya pingamizi kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) itatolewa ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe uamuzi ulipotolewa.

Mamlaka inaweza kuongeza muda wa kuwasilisha pingamizi usiozidi siku saba baada ya kuombwa na kupewa sababu za kutosha.

(3) Pale ambapo Mamlaka itapokea taarifa ya pingamizi kama ilivyoainishwa katika kanuni ndogo ya (1), itateua mtu wa kushughulikia pingamizi hilo.

(4) Mtu aliyeteuliwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (3) atapanga utaratibu utakaofuatwa kwa kuzingatia uzito wa pingamizi lolote.

(5) Mtu aliyeteuliwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (3) atapaswa kuzingatia maelezo ya pingamizi yaliyoandikwa au ya mdomo yaliyotolewa na mmiliki, mwingizaji au msafirishaji wa dawa katika kushughulikia pingamizi lake, na atatoa mapendekezo kwa Mamlaka.

(6) Mapendekezo yatakayotolewa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (5) yatawasilishwa kwa maandishi kwa Mamlaka, na nakala kwa mtoa pingamizi au mwakilishi wake aliyemteua.

(7) Mamlaka itazingatia mapendekezo yoyote yaliyofanywa kwa kufuata kanuni ndogo ya (5).

(8) Mkurugenzi Mkuu atamjulisha ndani ya siku kumi na nne mmiliki, mwingizaji au mtengenezaji wa dawa endapo anakubali mapendekezo yaliyotolewa kwa kufuata kanuni ndogo ya (5); pale ambapo hakubaliani atatoa sababu za uamuzi huo.

(9) Maamuzi ya Mamlaka yataendelea kutekelezwa mpaka pale itakapoamriwa vinginevyo wakati wa ushughulikiaji wa pingamizi hilo-

Rufaa

16.- (1) Bila kujali masharti ya kanuni ya 15, mtu yeyote ambaye hakuridhika na uamuzi wa Mamlaka anaweza, ndani ya siku sitini tangu kupata nakala ya uamuzi, kukata rufaa kwa maandishi kwa Waziri.

(2) Mrufani atawasilisha nakala ya rufaa kwa Mamlaka, ambapo ndani ya siku kumi na nne tangu kupata nakala ya uamuzi Mamlaka itajibu kwa maandishi kwa Waziri na kumpa nakala ya majibu mrufani.

(3) Pale ambapo Waziri ana maoni kwamba kuna hoja ya kujibu, anaweza kuwaita wahusika kupata taarifa zaidi au kufanya uamuzi wa kuruhusu au kutupilia mbali rufaa.

Makosa na

17.- Mtu yeyote anayekiuka au anayeshindwa kufuata Kanuni hizi moja

adhabu

kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja kumsaidia mtu mwingine kufanya kosa chini ya Kanuni hizi atakuwa na kosa na akitiwa hatiani, atapewa adhabu iliyowekwa kwa mujibu wa Sheria.

Kufifilisha makosa

18.- (1) Mkurugenzi Mkuu, Mkaguzi au mtu mwingine yeyote aliyeidhinishwa anaweza, kwa kufuata na kwa mujibu wa masharti ya Kanuni hizi, ikiwa ataridhika kwamba mtu ametenda kosa dhidi ya Kanuni hizi, atafifilisha kosa hilo kwa kupokea kutoka kwa mkosaji kiasi cha fedha ambacho kosa limetendwa.

(2) Kiasi cha fedha kitakacholipwa chini ya kanuni ndogo ya (1) kitakuwa ni theluthi mbili ya kiwango cha juu cha faini kwa kosa hilo kama ilivyoainishwa katika Sheria.

(3) Mamlaka ya kisheria yaliyotolewa na kanuni hii yatatumika pale ambapo mtuhumiwa atakiri kwamba ametenda kosa na anakubali kwa maandishi katika fomu ya kufifilishia makosa iliyoainishwa katika Kanuni za ada na tozo zinazotumika wakati huo.

(4) Mkurugenzi Mkuu au mkaguzi aliyepewa mamlaka ya kisheria chini ya kanuni hii atatoa risiti baada ya kupokea malipo kutoka kwa mtu anayelipa kiasi cha fedha chini ya kanuni ndogo ya (2).

(5) Kiasi cha fedha chini ya kanuni hii kitalipwa kwa Mamlaka.

(6) Mtu yeyote akishitakiwa mahakamani kwa kosa lolote dhidi ya Kanuni hizi, itakuwa utetezi endapo mtu huyo atathibitisha kuwa kosa analoshitakiwa nalo limefifilishwa chini ya kanuni hii.

MAJEDWALI

JEDWALI LA KWANZA

	FOMU YA OMBI LA KUTEKETEZA DAWA ZISIZOFAA	TMDA Tanzania Medicines & Medical Devices Authority

(Imetengenezwa chini ya Kanuni ya 11 (1))

Mimi / Sisi …………………………………….wa (anuani ya posta) tunaomba kuteketeza dawa zisizofaa kama zilivyoainishwa katika orodha iliyoambatishwa.

Anuani ya eneo jengo lilipo …………………. ………………….

Jina la msimamizi /mhusika……….. Namba ya usajili *(inapofaa)*…………

Sababu za kuteketeza ………………………………. ……………………………….

Thamani ya dawa katika soko (kwa TZS) ……………………………………….

Tamko:
Ninathibitisha kuwa taarifa nilizotoa katika fomu hii ni za kweli na sahihi

Tarehe ya maombi …………… Saini ya mwombaji……………muhuri……

Kwa matumizi ya Ofisi tu:

Imepokelewa na ………………… saini… ………………………………………….

Muhuri …………………… Tarehe ……………………………………………

JEDWALI LA PILI

	FOMU YA UHAKIKI WA OMBI LA KUTEKETEZA DAWA ZISIZOFAA	

(Imetengenezwa chini ya Kanuni ya 12 (2))

Jina la mwombaji ……………… wa anuani ya posta........... anayefanya biashara ya dawa kulingana na kiambatisho

Anuani ya Mahali ……………………………………………… …….………

Uzito (Kilo) .... Thamani ya soko (kwa TZS) ………………… ………………………… ....……………………………………

Je! Dawa halisi zinalingana na orodha iliyowasilishwa TMDA? NDIYO / HAPANA

Taarifa nyinginezo ………………………………………………………………………………………

………

…………………………… …………

Jina la mwombaji ……………………………….. Saini ………………………… ………

Tarehe ya uhakiki ………………………………………………………………………………

1. Jina la Mkaguzi wa Dawa……………………… Saini ……………………….

2. Jina la Mkaguzi wa Dawa ………………….. Saini …………………………

JEDWALI LA TATU

	REJESTA YA DAWA ZISIZOFAA	

(Imetegenezwa chini ya kanuni ya Kanuni ya 13(2 (a)))

Na.	Tarehe	Jina la Dawa		Nguvu ya dawa (pale inapofaa)	Muundo wa dozi	Ukubwa wa pakiti	Idadi	Namba ya toleo (inapobidi)	Thamani (TZS)	Sababu ya kutofaa	Tarehe ya kuteketeza
		Jina la kibiashara	Jina halisi								

JEDWALI LA NNE

	FOMU YA KUTEKETEZA	TMDA Tanzania Medicines & Medical Devices Authority

(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 14 (2)

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba inathibitisha kuwa imesimamia uteketezaji wa dawa zisizofaa (kama zilivyoorodheshwa katika kiambatisho) zinazomilikiwa na ……………………………. wa sanduku la posta …………………………………..

Uteketezaji ulifanyika katika (eneo au tanuru ambako dawa ziliteketezwa) …………………… Tarehe ……………………

Kwa njia zifuatazo za uteketezaji:-

1. …………………………………….
2. …………………………………….
3. ……………………………………

Uzito wa jumla ya dawa zilizoteketezwa ni ………………………… (Kilo) na thamani yake ni ………………………. (TZS)

Majina, vyeo na saini za wakaguzi na wasimamizi wengine:-

Jina	Cheo/Nafasi	Saini na Tarehe
1.		
2.		
3.		
4.		

Jina ____________________ Saini ya mmiliki/mwakilishi wake ___________________ Tarehe ________________

JEDWALI LA TANO

	CHETI CHA UTEKETEZAJI	TMDA Tanzania Medicines & Medical Devices Authority

(Imetengezwa chini ya Kanuni ya 14 (3)

Kumbukumbu Namba …………………………… **Tarehe ………………………………**

Mimi mwenye mamlaka ya usimamizi wa Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba Sura 219 inayohusika na udhibiti wa dawa, ninathibitisha kuwa dawa zisizofaa zinazomilikiwa na …………………………………… wa sanduku la posta ………………………………….. zimeteketezwa tarehe ………………………………….

Shehena tajwa iliteketezwa kwa ……………………………………………. (njia ya uteketezaji) katika …………………… (eneo au tanuru) chini ya usimamizi wa Mkaguzi wa Dawa, Afisa Afya, Afisa Afya Mazingira na Askari Polisi na mmiliki/mwakilishi wa mmiliki kama ilivyotajwa katika fomu namba ………………………… iliyoambatishwa.

Uzito wa shehena iliyoteketezwa ni ……………………… (kilo) na thamani yake ni …………………. (TZS)

…………………………………………… …………………………………………

Kny: Mkurugenzi Mkuu Saini na Muhuri

Dodoma,

……. …………….., 2021 *Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto*